# Tathmini Kuhusu Sera na Dhamira ya Ujamaa Nchini Tanzania

Abel Nyamahanga
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha
nyamahangaa@yahoo.com

**MAKALA HALISI**

**HISTORIA YA MAKALA**

**Kupokelewa:**12 Agosti 2021

**Kurekebishwa:** 30Sept. 2021

**Kukubaliwa:** 28 Oktoba 2021

**Kuchapishwa:** 08 Dis. 2021

ISSN: 2453 – 6016

Juzuu 7,

Toleo 2,

pp. 74 – 79.

**NUKUU:** Nyamahanga, A. (2021). Tathmini Kuhusu Sera na Dhamira ya Ujamaa Nchini Tanzania. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, *7*(2), 74 – 79.

**Ikisiri**

Makala hii imechunguza sera na dhamira ya ujamaa nchini Tanzania. Data za msingi zilizotumika katika makala haya zilipatikana maktabani kwa mbinu ya usomaji makini. Matini mbalimbali zilichunguzwa ili kupata data za msingi. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika makala hii umeongozwa na nadharia ya Uhalisia. Matokeo katika makala hii yanaonesha kuwa misingi ya sera za Azimio la Arusha na ujenzi wa Ujamaa wa Tanzania ulikabiliwa na masuala mbalimbali yaliyoathiri utekelezaji wake. Mkakati wa kuwahamisha wananchi kwa nguvu katika vijiji vya maendeleo ulipingana na haki za binadamu kwa kuwa baadhi ya viongozi walitumia nguvu kupita kiasi. Pia, uliathiri kilimo cha mazao ya kudumu ya biashara katika baadhi ya mikoa. Azimio la Arusha lilionekana kuwa ni sera iliyoshindwa kufanya kazi na kuleta maendeleo. Makala hii inahitimisha kuwa Azimio la Arusha lilifumbata itikadi, dira na mwongozo wa taifa. Azimio la Arusha lilihitaji kufanyiwa marekebisho ili liendane na mazingira ya sasa ya ulimwengu badala ya kulitupa kabisa. Tatizo kubwa lililopo sasa ni kwamba kila awamu ya uongozi unakuwa na mtazamo na mwelekeo binafsi wa kuendesha nchi.

**Maneno Msingi:** Azimio la Arusha, Sera za Azimio la Arusha, Dhamira za Azimio la Arusha na Ujamaa wa Tanzania.

## Utangulizi

TANU, chama cha siasa cha awali nchini Tanzania, kilikuwa na shabaha ya kuwa na serikali ya Ujamaa. Hali halisi ya siasa ya Ujamaa ilitolewa wakati wa Azimio la Arusha, ambapo halmashauri ya TANU ilikutana Arusha na kuandaa siasa hiyo; na kutangazwa Februari 5, 1967. Msisitizo mkubwa katika Azimio hilo ulikuwa ni Uhuru na Maendeleo ya Mtanzania (TANU, 1967). Lengo la TANU lilikuwa ni kujenga nchi ya Kijamaa na kufanya mabadiliko ya siasa, uchumi na mfumo wa jamii mara baada ya kupata uhuru. Pia, kililenga kuunda falsafa ya ujenzi wa taifa jipya. Ujamaa uliokusudiwa kujengwa ulielezwa namna misingi yake katika maisha ya kijadi ya jamii za Waafrika. Jamii hizo zilikuwa zikiishi pamoja katika vijiji na koo

kijamaa. Walifanya kazi pamoja kwa kusaidiana na kushirikiana. Jamii hizo hazikuwa za kitabaka. Chama cha TANU kilirejelea mfumo wa kijadi ili kujenga Ujamaa wa kitaifa nchini Tanzania.

Demokrasia ilikusudia kujengwa katika misingi ya jadi za Waafrika. Katika jamii hizo mifumo ya kisiasa ilikuwa ya kushirikiana na kukubaliana (Nyerere, 1962). Mfumo huu haukuwa wa siasa za ushindani. Wazee walikuwa wakijadiliana na kufikia maamuzi ya msingi ya kuendesha shughuli za jamii kwa utaratibu maalumu. Baada ya kupata uhuru ilipendekezwa kujenga misingi ya demokrasia ya Kiafrika. Utaratibu huo ulipaswa kujengwa chini ya mfumo wa chama kimoja. Falsafa hii ilifuatwa na viongozi wengi wa nchi za Kiafrika zilizokuwa zimepata uhuru. Tanzania na baadhi ya nchi za Kiafrika ziliamua kufuata mfumo wa chama kimoja. Katika misingi ya demokrasia ya Kiafrika, wananchi na wanachama wote ndio washike hatamu na kufanya maamuzi. Misingi hiyo ilikuwa ni sehemu ya Azimio la Arusha lililolenga kuhakikisha usawa, haki, heshima, utu na maendeleo ya binadamu (Nyerere, 1974). Chama kilipinga Ujamaa wa kisayansi, ambao licha ya kuwa na chama kimoja, viongozi wachache walioshika hatamu na kufanya maamuzi.

Azimio la Arusha lilitokana na mabadiliko ya jamii kabla ya Azimio la Arusha mwaka 1967. Badiliko kubwa lilikuwa ni kukua haraka kwa matabaka baina ya wananchi. Sera ya serikali ya kugawa madaraka serikalini kwa Waafrika kutoka kwa Wazungu iliwafanya baadhi yao kutumia nafasi zao kutajirika haraka. Walijitokeza wafanyabiashara na viongozi wa Kiafrika waliotajirika haraka. Mabadiliko hayo yalisababisha pengo baina ya matajiri wachache na maskini wengi kuongezeka (Pratt, 1968). Licha ya kukua kwa matabaka, miradi mikubwa ya uchumi, makampuni makubwa ya biashara na mabenki, viwanda na njia kuu za uchumi zilikuwa bado zinamilikiwa na Wazungu na Waasia. Nia ya Azimio ilikuwa njia ya kuondoa mfumo wa matabaka katika jamii na kuhakikisha kuwa njia za uzalishaji mali na uchumi zinamilikiwa na wananchi. Makala hii inachunguza sera na dhamira ya Azimio la Arusha na Ujamaa wa nchini Tanzania.

**Dhamira ya Azimio la Arusha na Ujamaa wa Tanzania**

Wananchi wengi waliunga mkono Azimio la Arusha kwa kuwa maudhui yake yalilenga na kusisitiza ubinadamu, utu na uraia wa Watanzania. Baadhi ya mambo yaliyotiliwa mkazo ni usawa, haki za binadamu, haki ya raia kumiliki na kushiriki katika mambo ya uchumi, haki ya kuwa na maisha bora na kujenga misingi ya demokrasia na utawala bora. Pia, lilisisitiza umuhimu wa kuwa na sera bora za mambo ya nje ikiwa ni pamoja na kushiriki ukombozi wa bara zima la Afrika (Mihambo, 2013). Sehemu kubwa ya dhamira ya Azimio la Arusha ni sera ya kujitegemea. Kujitegemea ni pamoja na kuepukana na fikra potofu za kutegemea fedha na misaada kutoka nje kwa shughuli za maendeleo. Msingi mkuu wa maendeleo ni kufanya kazi kwa bidii. Uhuru na kazi. Mambo mengine ya msingi kuhusu maendeleo ya taifa ni ardhi, siasa safi, uongozi bora na watu. Msingi wa ujamaa ulikitwa katika mambo yaliyoelezwa katika sehemu hii.

**Kujenga Demokrasia na Kuondoa Unyonyaji**

Katika nchi ya kijamaa kila mtu ni mkulima ama mfanyakazi. Mfumo huu hauna makabaila wala mabepari, kufanyiwa kazi na kutumikishwa (Mapolu, 1976). Kila mwenye afya ya kufanya kazi, afanye kwa juhudi na maarifa. Kila mtu apate haki ya jasho lake isipokuwa watoto wadogo, vikongwe, walemavu na wagonjwa. Hata hivyo, inaaminika kuwa bado Tanzania haijafikia ujamaa kamili kuwa sababu dalili za ubepari na ukabaila zipo. Nchi ya Kijamaa haipaswi kuwa alama zozote za mfumo wa kibepari au kikabaila. Nchi ya kijamaa haiwezi kuwa ya kijamaa kwa vile njia zote za uchumi na uzalishaji mali zimo mikononi mwa umma. Demokrasia ni muhimu katika ujamaa, uchaguzi wa viongozi wa chama na serikali hauna budi kuwapo (Mniwasa & Shauri, 2001). Uwapo wa demokrasia unamaanisha kuwa serikali inatakiwa itokane na wafanyakazi na wakulima kwa njia ya uchaguzi huru na halali. Demokrasia ina maana kuwa hakuna mfumo wa ukandamizaji wa siasa.

**Kujenga Misingi Imara ya Ujamaa**

Ujamaa ni njia mojawapo ya kuishi. Ujamaa unaweza kujengwa na watu wanaoamini katika misingi ya Ujamaa. Watu hao wanapaswa kuutazama Ujamaa kama sehemu ya maisha yao. Ujamaa wa Tanzania ulipaswa kujengwa na watu wenye imani, moyo wa kutenda na kufuata misingi ya Kijamaa (Nyerere, 1968). Wote wenye imani ya Kijamaa ni wale wote katika Afrika na kwingineko ambao hawataishi kutegemea jasho la wengine wala kufuata tabia na matendo ya kibepari na kikabaila. Wananchi na viongozi wasio na imani ya Kijamaa hawawezi kufuata misingi ya Kijamaa. Maisha na matendo yao hayawezi kuwa ya Kijamaa. Tanzania inajaribu kufuata mbinu za kuinua hali za watu Kijamaa licha ya kuwapo kwa changamoto lukuki katika kipindi hiki cha mfumo wa soko huria na vyama vingi vya siasa.

Kisiasa, Azimio la Arusha lilikuwa ni dira na itikadi ya kitaifa iliyowaunganisha wananchi na kupata umoja imara wa kitaifa na kudumisha amani. Tanzania iliweza kujenga demokrasia ya mfumo wa chama kimoja na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga misingi ya usawa. Kila baada ya miaka 5 kulikuwa na uchaguzi mkuu na kuunda serikali inayotokana na wananchi. Muundo wa uongozi uliwaruhusu wananchi walikuwa wanakutana na kujadili mambo yao kidemokrasia. Kiuchumi, ilikuwa rahisi kwa wataalamu kuwafikia wakulima na kuwaelimisha kuhusu mbinu za kisasa na matumizi ya teknolojia ya kuendeleza kilimo cha kisasa (Shivji, 1970). Matokeo ya kiuchumi yalijitokeza katika ujenzi wa viwanda na kupanuliwa kwa reli ya TAZARA, bandari, barabara na shirika la ndege. Huduma za jamii kitaifa, hospitali na shule ziliongezeka. Kila kijiji kilikuwa na angalau na shule moja ya msingi. Zahanati na vituo vya afya viliongezeka. Vijiji vingi viliishapata maji safi ya bomba na kuwa na nyumba za kisasa.

**Kudhibiti Njia Kuu za Uchumi**

Kujitegemea kiuchumi kunahitaji juhudi na maarifa. Katika nchi ya Kijamaa, njia kuu za uzalishaji mali na uchumi zinatakiwa ziwe chini ya umiliki na udhibiti wa wafanyakazi na wakulima. Umiliki na udhibiti huo unafanywa na dola na vyama vya ushirika kwa niaba ya makundi hayo (Mpangala na wenzake, 2019). Njia muhimu za uchumi ni mashamba makubwa, madini, benki, bima, mafuta na umeme, maduka ya

jumla, viwanda na chochote kinachotegemewa na umma katika maisha yao ya kila siku. Pia, lazima iwe wazi kuwa chama kinachotawala ni chama cha wafanyakazi na wakulima. Chama cha TANU kulitimiza wajibu huo wa kuwa chama wafanyakazi na wakulima wadogo wadogo.

**Sera za Azimio la Arusha na Ujamaa wa Tanzania**
Azimio lilitangazwa mwaka 1967. Tangu kuasisiwa mpaka kufikia mwaka 1970 kilikuwa ni kipindi cha maandalizi. Utekelezaji hasa ulianza mwaka 1971 mpaka 1985, kipindi cha miaka 15 tu. Utekelezaji wake ulichukua muda mfupi sana kuweza kuufanyia tathmini yakinifu kuhusu mafanikio na matatizo yake. Utekelezaji wa Azimio la Arusha ulifanywa kwa kurejelea sera kuu tatu kama zilivyofafanuliwa katika sehemu hii.

**Kuhimiza Ujamaa na Maendeleo Vijijini**
Lengo kuu la sera hii lilikuwa ni kuhakikisha kuwa kuna maendeleo ya uchumi na huduma za jamii vijijini ili kutokomeza umaskini, umaskini na maradhi (Ogenga, 2015). Mkakati uliofanyika ulikuwa ni kuanzishwa kwa vijiji vya Ujamaa na vijiji vya maendeleo. Kuanzia mwaka 1968 hadi 1973 mkazo ulikuwa kuwashawishi wananchi kujiunga na vijiji vya Ujamaa kwa hiari yao. Katika vijiji vya Ujamaa, wanavijiji walihitaji kuishi maisha ya Kijamaa. Serikali ilibuni mbinu mpya ya kuanzisha vijiji vya maendeleo badala ya vijiji vya Ujamaa. Pia, iliwalazimisha wanavijiji kuvihama vijiji vyao vya asili na kujiunga na vijiji vya maendeleo vilivyopangwa na kupimwa na serikali. Matokeo yake ni kwamba kulikuwa na ongezeko kubwa na la haraka la watu waliohamia kwenye vijiji hivyo vya maendeleo.

**Kutaifisha Njia Kuu za Uchumi**
Utaifishaji ulilenga kuhakikisha kuwa njia kuu za uzalishaji mali na uchumi zinakuwa mikononi mwa wafanyakazi na wakulima kupitia njia ya dola na vyama vya ushirika. Utekelezaji wa jambo ulihusu utaifishaji wa mashamba ya walowezi, makampuni makubwa ya biashara, viwanda na njia kuu za uchukuzi na mawasiliano, hasa bandari, shirika la posta na simu, shirika la ndege na njia za reli (Mpangala & Mawazo, 2015). Njia zote zilizotaifishwa zilifanywa kuwa mashirika ya umma. Licha ya ubinafsishaji uliokwishafanyika katika mashirika hayo, kulikuwa na changamoto kubwa kwa upande wa usimamizi na uendeshwaji wake. Baadhi yake yaliendelea kudhoofika badala ya kustawi zaidi.

**Kuimarisha Elimu ya Kujitegemea**
Lengo la sera ya Elimu ya Kujitegemea lililenga kuwezeshe kukuza imani ya usawa wa binadamu ili kukuze fikra za kufanya kazi kwa pamoja kwa manufaa ya wote. Pia, iwaandae vijana kujiona kuwa wao ni sehemu kamili ya jamii wanamoishi na kuwawezesha kukuza vipawa vya kudadisi, kukosoa na kujenga fikra na hali ya kujiamini. Elimu iliyotolewa ilipaswa kuwaandaa vijana kupenda na kuwa tayari kuishi vijijini ambako wananchi wengi wanaishi. Katika utekelezaji wa malengo hayo, serikali ilitaifisha shule zote za msingi na sekondari za watu binafsi na za mashirika ya dini na kuwa shule za serikali. Utaifishaji uliiwezesha serikali kujenga

mazingira ya kutoa nafasi sawa ya kupata elimu ya msingi na sekondari bila kujali tofauti zao za dini. Serikali iliweza kufanya mabadiliko ya mitaala ya elimu ya msingi na sekondari na kuhakikisha masuala ya elimu ya kujitegemea yanakuwa sehemu ya mitaala hiyo kinadharia na kivitendo (Lema na wenzake, 2006). Kila shule ilianzisha shughuli za kujitegemea za kufanywa kutegemeana na mazingira ya shule inayohusika kama vile kufuga na kulima.

**Hitimisho**

Misingi za sera za Azimio la Arusha na ujenzi wa Ujamaa wa Tanzania ulikabiliwa na masuala mbalimbali yaliyoaathiri utekelezaji wake. Mkakati wa kuwahamisha wananchi kwa nguvu katika vijiji vya maendeleo ulipingana na haki za binadamu kwa kuwa baadhi ya viongozi walitumia nguvu kupita kiasi. Uhamishaji huo uliathiri kilimo cha mazao ya kudumu ya biashara katika baadhi ya mikoa. Pia, kupanda ghafla kwa mafuta katika nchi za Kiarabu mwaka 1973 na mwaka 1979 kuliathiri uchumi wa nchi changa. Hali hiyo iliathiri uzalishaji na kushuka kwa bei ya mazao ya biashara katika soko la dunia (Laeven & Valencia, 2013). Tanzania kukataa kufanya marekebisho ya uchumi ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa kuanzia mwaka 1979 hadi 1985 ilipata pigo lililotokana na Benki ya Dunia kuzizuia nchi tajiri kutoa misaada. Hali hii iliifanya Tanzania kuwa katika hali mbaya zaidi ilipofikia mwaka 1985. Mwaka 1986 Tanzania ililazimika kukubaliana na masharti na kuanza harakati za kufufua uchumi. Msingi mkuu wa masharti ulilenga kuupokea mfumo wa ubepari ambao ni kinyume cha mfumo wa Ujamaa.

Katika kipindi cha miaka 15 tu, Azimio lilikabiliwa na matukio mengi yaliyoathiri utekelezaji sera na misingi yake. Tukio mojawapo ni kuvunjika kwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika Mashariki mwaka 1977. Anguko hili liliilazimisha serikali kutumia fedha nyingi zilizoigharimu kwa kuyaimarisha mashirika yote yaliyokuwa chini ya EAC kama vile Shirika la Bandari, Shirika la Reli, Shirika la Ndege, Shirika la Posta na Mawasiliano (Mpangala, 2000). Mwaka 1978, Rais wa Uganda, Iddi Amini, aliamuru majeshi yake kuivamia Tanzania sehemu ya Kagera. Tanzania ililazimika kutangaza vita iliyoisha mwaka 1979. Licha ya kuwa Tanzania ilishinda, lakini ilitumia gharama kubwa, ukitilia maanani kuwa kipindi hicho kilikuwa cha matatizo makubwa ya kiuchumi. Mambo hayo yote yalichangia kwa kiasi kikubwa kufifia kwa utekelezaji wa dhamira ya Azimio la Arusha.

Kifo cha Azimio la Arusha kilitokana na Azimio la Zanzibar mwaka 1991 lililoamua kuachana na Azimio la Arusha. Azimio la Arusha lilionekana kuwa ni sera iliyoshindwa kufanya kazi na kuleta maendeleo. Kuanguka kwa Azimio kulisababishwa na matatito ya uchumi wa dunia na kwa Tanzania yalizidishwa na ukame, kusambaratika kwa Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki, vita ya Kagera na kubanwa na Benki ya Dunia (Nyagetera, 1995). Tanzania iliachana kabisa na ujenzi wa Ujamaa na kuanza kujenga mfumo wa jamii wa kibepari. Kipekee, Azimio la Arusha lilifumbata itikadi, dira na mwongozo wa taifa. Lilihitaji kufanyiwa marekebisho ili liendane na mazingira ya sasa ya ulimwengu badala ya kulitupa

kabisa. Nchi haina dira na mwongozo wa kitaifa kwa sababu kila Raisi anakuwa mwelekeo binafsi wa kuendesha nchi.

**Marejeleo**


Lema, E., & Wenzake. (2006). *Nyerere on Education: Selected Essays and Speeches 1967 – 1997*. Dar es Salaam: Haki Elimu.

Mapulo, H. (1976). *Workers and Management*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mihanjo, A. (2010). *Falsafa na Ufunuo wa Maarifa*. Morogoro: Salvatorianum.

Mniwasa, E., & Shauri, V. (2001). *Review of the Decentralization Process and It's Impact on Environmental and Natural Resources Management in Tanzania* (p.27). Lawyers' Environmental Action Team.

Mpangala, P. G. (2000). *Major Issues in Tanzanian Economic History Part 2: Transformation of Peasant Agriculture for Hundred Years, 1891 – 1990*. Dar es Salaam: TUKI.

Mpangala, P. G., & Mawazo, R. R. (2015). *Historia ya Mkombozi, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere*. Dar es Salaam: TUKI.

Mpangala, P. G., & Wenzake. (2019). *Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Maendeleo*. TUKI: Chuo Kikuu cha Tanzania.

Nyagetera, B. M. (1995). Inestment, Foreign and Self-Reliance in Tanzania: A State ot the Art Review. ESRF Discussion Paper Series, No. 001.

Nyerere, J. K. (1962). *Tujisahihishe*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nyerere, J. K. (1968). *Freedom and Development*. Oxford University Press.

Nyerere, J. K. (1974). *Binadamu na Maendeleo*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Ogenga, O. (2015). Mwalimu Julius Kambarage Nyerere's Philosophy. Contribution and Legacy. *African Identities*, 13: 1 – 18.

Pratt, C. (1999). Julius Nyerere: Refrections on the Legacy of Socialism. *Canadian Journal of African Studies*, Vol. 33, No. 1: 133 – 139.

Shivji, I. G. (1970). *Tanzania: Silent Class Struggle*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

TANU (1967). Azimio *la Arusha: Ujamaa na Kujitegemea*. Dar es Salaam: Reprinted by Haki Elimu 2010.